

Ebrahim Hussein
1980 (1967)
ALIKIONA¹
Nairobi: East African Publishing House

Nacherzählt von
Lourenco Noronha

Lektor (1974-2009) für Swahili-Literatur
am
Institut für Afrikawissenschaften der Universität Wien
Taasisi ya Taaluma ya Bara la Afrika
Chuo Kikuu cha Vienna

Stand: Mai 2009

¹ Hussein, Ebrahim. 1970. Michezo ya Kuigiza. Nairobi: East African Publishing House. S. 43-64.

Widmung
Kutabaruku

al-hamdu li-llahi
subhanahu wa-ta'ala

1. Einleitung
Utangulizi

1.1. Autor: Biographische Notizen
Wasifu ya mtunzi

Ebrahim Hussein wurde 1943 in Lindi geboren. Er besuchte die *Aga Khan Secondary School* in Dar-es-Salaam, studierte von 1966 bis 1969 Literatur, Französisch, Soziologie und Theaterwissenschaft an der dortigen Universität. 1969 war er wissenschaftlicher Assistent am *Department of Theatre, Arts, and Music* der Universität Dar-es-Salaam und seit 1970 wissenschaftlicher Aspirant an der Humboldt-Universität zu Berlin, wo er in Theaterwissenschaft promovierte. Seine Dissertation, datiert 1971, hat den Titel The Development of Drama in East Africa. 1978 kehrte er an die Universität Dar-es-Salaam zurück und lehrte am *Department of Theatre, Arts, and Music*. (Ich bin auf der Suche nach weitere Information.)

1.2. Thematische Einführung.
Kiini (dhamira, dhana, mada, wanda/ma-) maalum

Alikiona gehört zu den zwei ersten Theatertexten, die Ebrahim Hussein 1967 in Darlite, der literarischen Zeitschrift der Universität Dar-es-Salaam, veröffentlicht hat. Für Hussein, der ein ideologisch engagierter Autor ist, kann man diesen Text nicht als typisch betrachten. Der Text liegt aber durchaus im damals noch üblichen Trend einer Kombination von *kichekesho*² und *maadili*³. Das Verhaltensmuster von Saida und Omari in *Onyesho la Tatu* entspricht vielleicht einer lokalen Variante der 60er Jahre des vergangenen Jahrhunderts. Die Handlung ist übersichtlich. Es geht um die Geschichte einer Frau, die neben ihrem Ehemann einen Liebhaber hat. Der Schluß geht von einer selbstzerstörerischen Aussage der Ehefrau aus und der Ehemann behält sich das Recht vor, die Gattin auf Grund ihrer ehelichen Untreue mit einem dreifachen Spruch „*Talaka, Talaka, Talaka*“ zu entlassen. Der Theatertext lässt diese Entscheidung offen. Eine Entlassung in der umgekehrten Richtung war nicht üblich.⁴ Der Theatertext lässt diese Entscheidung offen.

In Tansania gilt inzwischen ein neues Ehegesetz genannt Sheria Mpya ya Ndoa. Die Eheschließung nach christlichem und islamischem Recht vor einem vereidigten Vertreter dieser Religion ist weiterhin staatlich anerkannt. Sie muß aber beim Standesamt angemeldet werden.

Kichekesho, eine Variante von „Volksbelustigung“ wird in Swahili-Theatertexte eingebaut. Gewöhnlich kommen in diesem Kontext Inder mit mangelnder Sprachkompetenz, die asozial dargestellt werden, oder „Tratschweiber“ vor. In diesem Theatertext sind die „Tratschweiber“ durch Saida und Mama Pili vertreten. Abdallah in

2 Humor

3 Gutes (gerechtes) Benehmen.

4 Frau Zainab Omar aus Sansibar, ehemalige Lektorin am Institut für Afrikawissenschaften der Universität Wien, sagte mir, daß ein islamischer Ehemann seiner Ehefrau ein *Talaka* geben kann, die Ehefrau darf aber um ein *Talaka* bitten.

Siehe auch: Hanak, Irmi. 1996. „Language, Gendre and Law: Divorce in the Context of Muslim Family Law in Zanzibar“, in: Journal of African Cultural Studies. London: SOAS. 9/1, S. 27-42. (Z.7.32.9/1.).

seinem Versteck unter dem Bett trägt seinerseits zum Aspekt „*Kichekesho*“ bei.

Schon in diesem ersten Theatertext erkennt man Hussein's kompakte und eindrucksvolle Sprache sowie eine zwingende Darstellung von Personen, die ihn zu einem bedeutenden Autor der frühen Swahili-Theatertexte macht.

1.3. Literaturhinweise.

Marejeo

Die Zahlen in Klammern entsprechen der Signatur der Fachbibliothek der Afrikawissenschaften und Orientalistik der Universität Wien.

1.3.1. Primärliteratur

- Fiebach, Joakim (ed.). 1974. Stücke Afrikas (In deutscher Übersetzung: Hussein, Ebrahim. Kinjeketile. Ramadhani, John. Streik in Mazinde). Henschel Verlag.
- Hussein, Ebrahim. 1981 (1969). Kinjeketile. Nairobi: OUP. 49pp. (B.8.9.26.).
- Hussein, Ebrahim. 1970. Michezo ya Kuigiza (Wakati Ukuta & Alikiona). Nairobi: EAPH. 64pp. (B.8.9.7.).
- Hussein, Ebrahim. 1987 (1971). Mashetani. Dar es Salaam: OUP. 57pp. (B.8.9.27/1.).
- Hussein, Ebrahim. 1975 (1971). Wakati Ukuta. Nairobi: EAPH. 41pp. (B.8.9.4.).
- Hussein, Ebrahim. 1976. Jogoo Kijijini & Ngao ya Jadi. Nairobi: OUP. 50pp. (B.8.9.55.).
- Hussein, Ebrahim. 1984 (1980). Arusi. Nairobi: OUP. 50pp. (B.8.9.25.).
- Hussein, Ebrahim. 1982. Jambo la Maana. Dar es Salaam: Africana Publishers. 28pp. (B.8.14.20.).

1.3.2. Sekundärliteratur

- Hussein, Ebrahim N. 1980. "Traditional African Theatre", in: Schild, Ulla. The East African Experience. Berlin: Reimer, S. 35-53. (S.6.6.1.).
- King'ei, Godfrey K. 1987. "Usanifu wa Lugha katika Uandishi wa Ebrahim Hussein", in: Mulika. Dar es Salaam: IKR. 19, S. 19-35. (Z.1.11.19.).
- Mmbago, Nathaniel. „Msingi wa Michezo ya Kuigiza: Michezo ya Ebrahim Hussein“, in: Mulika. Dar es Salaam: IKR.
- Mugo, Micere Githae. 1976. "Gerishon Ngugi, Penina Muhando and Ebrahim Hussein. Plays in Swahili", in: African Literature Today. London: Heinemann. 8, S. 137-141. (Z.3.1.8.).
- Sengo, Tigiti. 1975. „Ebrahim Hussein. Mwandishi wa Michezo ya Kuigiza“, in: Hisi Zetu. Dar es Salaam: IKR. 2, S. 58-95. (Z.1.35/2.).

2. Texte
Matini

2.1. Personen
Wahusika

Omari: Ein Mswahili
Saida: Ehefrau Omaris
Abdallah: Der Liebhaber Saidas
Mama Pili: Nachbarin Saidas
Mama Tatu: Nachbarin Saidas
Abudu: Ein Bekannter Omaris

2.2. Theatertext
Tamthilia

2.2.1. Onyesho la kwanza

Auf der Bühne stehen ein Bett, ein Tisch und ein Sessel. Es ist dunkel. Nach einiger Zeit sieht man eine Frau, die vom Bett aufsteht, ein Kanga anzieht und mit dem Streichholz eine Lampe anzündet. Sie schaut auf ihre Uhr.

Saida: Mama! Saa mbili. Haraka haraka. Bwana ondoka, mume wangu atakuja sasa hivi.

Abdallah: (*Anavaa shati na viatu*) Bado. Haraka yote ya nini?

Saida: Hapana bwana, siku nyingine anakuja mapema. (*Abdallah anainuka kitandani*)

Saida: Ah bwana tafadhali (*Anamvuta mkono*). Hm tafadhali fanya haraka uende.

Abdallah: Niambie kwanza lini utakuja?

Saida: Kuja wapi?

Abdallah: Nyumbani!

Saida: Je mkeo utamweka wapi?

Abdallah: Mke wangu kasafiri, kwani wewe hujui?

Saida: Nijue ataniambia nani? Kwa kweli siwezi kuja.

Abdallah: Aaah.

Saida: Sivyoo hivyo.

Abdallah: Sivyoo hivyo namna gani?

Saida: Nitamwambia nini mume wangu? Nitamwambia kama ninakuja kwako?

Abdallah: Kama ungalikuwa unataka ungalitafuta njia. Wanawake mna maarifa namna kwa namna.

Saida: (*Anatazama saa*) Mama we! Nenda bwana. Sasa hivi atakuja.

Abdallah: Sasa utakuja?

Saida: Ndiyo ndiyo.

Abdallah: Unasema kwa dhati au kwa chati?

Saida: Mimi nimekwambia nitakuja nitakuja; tena nitakuja kukaa siku mbili.

Abdallah: (*Anacheka*) Unanifanya mtoto sana. Utamwambia nini mumeo mpaka akuachie kukaa kwa siku mbili.

Saida: Wewe unataka nini. Nimekwambia nitakuja nitakuja tu.

Abdallah: Lini?

Saida: Kesho.

Abdallah: Ah – (*Wanasikia mtu anakuja. Kiatu kinagonga*) (*Uk. 44-46*).

Abdallah und Saida vernehmen Stimmen von zwei Frauen, Mama Pili und Mama Tatu, die vor dem Haus plaudern. Abdallah versucht rasch durch die Nebentüre hinauszugehen, als er aber jemanden kommen hört, kehrt er zurück und versteckt sich schnell unter dem Bett. Die Zuschauer sehen ihn. Omari kommt herein.

Saida: (Anampokea mumewe huku anakifichaficha kitanda asitazame upande ule) Habari za kazini bwana?

Omari: Njema njema. (Anataka kukaa juu ya kiti. Akikaa juu ya kiti ataona mvungu wa kitanda).

Saida: Ah usikae hapo Bwana, kiti kibovu. Nikitaka kukipeleka kwa fundi lakini sikupata nafasi.

Omari: Kibovu?

Saida: Eh kibovu. (Omari anataka kukaa juu ya mkeka. Akikaa juu ya mkeka ataona mvungu wa kitanda).

Saida: Aah usikae juu ya mkeka. (Anamkamata mkono) Mkeka mchafu.

Omari: Mchafu? Mbona mimi nauona safi.

Saida: Mchafu sana.

Omari: Oh haya (anauangalia mkeka. Anatazama mkewe. Anataka kukaa juu ya kitanda).

Saida: Usikae juu ya kitanda. Ah basi kaa kaa (Anamkalisha. Omari anajitupa juu ya kitanda).

Abdallah: Aaah!

Saida: (Kusikia vile anajidai yeye ndiye alipiga kelele) Aaah! Aah! (Uk. 46-47).

Saida stellt sich krank und bittet ihren Ehemann, er möge sie ins Spital bringen. Er möchte wissen, was für Beschwerden sie hat.

Saida: Sasa afadhali kidogo. Kiuno hiki nacho kitaniua. Eh bwana kweli hebu twende uwani mara moja – kuna kitu kizuri nataka kukuonyesha.

Omari: Leo una nini wewe? Nakuona kama una kihaha kidogo.

Saida: Twende nje.

Omari: Kuna nini huko nje? Huoni kama nimetoka kazini. (Anajitupa kitandani)

Abdallah: Ah

Saida: Ah ah, mgongo huu utaniua, lazima niende hospitali. Nipeleke baadaye.

Omari: Ngoja nipumzike kwanza, nitakupeleka baadaye.

Saida: (Kwa hamaki ya uwongo) Unaona kupumzika kwako bora kuliko uzima wangu. Mimi mgonjwa ... aah mgonjwa unaniacha nife. Hunipendi tu mimi najua unao wako unaowapenda lakini siye mimi. Najua yote kwani mimi unafikiri sijui.

Omari: Hee! Una nini leo wewe?

Saida: Nina nini? Nimekwisha kukuambia kuwa ninakufa kwa ugonjwa. Bado nina nini tena? Kama hutaki sikusema tu?

Omari: Haya twende huko hospitali, twende. (Amesimama)

Saida: Usiniambie hivyo, kama hutaki basi. Kaa tu.

Omari: Mama mimi wewe! Sasa mimi jamani nimesema nini! Sikusema twende mimi, eh?

Saida: Ah hivyo ulivyosema. Kama ninakulazimisha vile.

Omari: Lahaula wee! Nikikataa, vita. Nikikubali ngondo, sasa nifanye nini? Hebu niambie mke wangu, nifanye nini, au niseme nini?

Saida: Aah (Ameweka shingo upande).

Omari: Basi mke wangu twende hospitali. Mimi tayari. (*Anamshika mkono*). Haya twende.
Saida: Ngoja nichukue buibui (baibui). (*Anachukua buibui juu ya mchango*). Tupite huku. (*Anaonyesha njia ya uani*)
Omari: Pita njia yoyote unayotaka. Twende. (*Wanatoka. Abdalla anatoka mvunguni, anatoka kwa mlango alioingilia Omari. Muda si muda, Omari na mkewe wanaingia*). (Uk. 48 - 50).

Nach einiger Zeit sind Omari und seine Ehefrau Saida wieder auf der Bühne. Sie waren gar nicht beim Arzt, denn Saida hat eine Ausrede gefunden, zurückzukehren. Sie entschuldigt sich, dass sie ihn belästigt hat, obwohl er müde ist. Sie hatte vergessen, daß sie bei Mama Pili einen Termin hat. Sie bittet ihren Mann auszuruhen, bis sie ihm das Essen bereitet hat. Omari ist zwar zu einer Koranlesung eingeladen, schafft es aber nicht hinzugehen, denn er ist müde. Er bleibt zuhause.

Saida: Je, unataka kitu?
Omari: Hapana, hapana. (*Analala juu ya kitanda. Mkewe anakuja kumkanda. Omari anashangaa, anatikisa kichwa hasemi kitu*).
Saida: (*Baada ya muda mchache*) Bwana eh!
Omari: Km!
Saida: Nataka kwenda nyumbani. (*Omari anageuka kumtazama mkewe*) Lakini sivyo unavyofikiria. Siku nyingi sijawaona wazee. Nipe ruhusa kesho na kesho kutwa nikawatazame wazee. Unajua siku nyingi sijawaona. Siku zile nilizo kwenda, kama nilivyokwambia, mama alikuwa mgonjwa gonjwa. Utu uzima tena. (*Anamkanda kimya*) Kama hutaki nende (niende) basi ...
Omari: Mke wangu mswalie mtume we, utanitoa roho. Hivyo nimekataa mimi hapa? (Uk. 50-51).

Er lässt sie tun, was sie will. Sie darf gehen heute, morgen oder sonst wann immer sie will. Inzwischen kommt Mama Pili etwas verspätet herein.

Mama Pili: Hodi hodi. (*Kutoka nje*). Hodi, hodi wenyewe.
Saida: Karibu, karibu. Mbona umechelewa babu wee? Nimekungoja wee - iih nikakata tamaa.
Mama Pili: Kazi ilionipata ndogo!
Saida: Kaa basi (*Anampa kiti*)
Mama Pili: Nitakaa babu na roho nitue. (*Omari anainuka kumpisha Mama Pili. Anaona ajabu kumwona mkewe anampa kiti "kibovu" mgeni. Lakini Saida kesha sahau*) Jee Habari (*anamwuliza Omari*) Habari za kazi?
Omari: Njema, njema. Jee nyumbani wote wazima?
Mama Pili: Hivyo hivyo tu, hakuchi kuna kucha.⁵
Omari: Ndiyo maisha (*Anavaa kanzu. Anataka kutoka*)
Saida: Ehe lete habari.
Mama Pili: Habari... kwanza nimekuletea sare hii ununue. (*Anampa kanga*)
Omari: (*Kusikia vile*) Mimi nitaondoka mara moja nitarudi sasa hivi. (*Anakwenda mlango upesi*)

5 Sprichwort: Hauchi-hauchi, unakucha. Es dämmert nicht, es dämmert nicht, es dämmert. *Bedeutung:* Auch wenn es scheint, dass die Nacht nie zu Ende geht, kommt der nächste Tag doch. Auch wenn eine Situation aussichtslos erscheint, solltest du nicht aufgeben. Eine Lösung wird kommen.

Saida: Basi umesikia hivyo nachukua hii sare.

Omari: Nimesikia mke wangu, nimesikia. (*Anatoka, lakini si kwa haraka kama mwanzo. Baada ya kutoka, Saida na Mama Pili wanatazana, wanacheka*).
(Uk. 51- 53).

Omari tut so, als ob er nichts gehört hätte. Die Frau kommt ihm scheinbar zu teuer. Er geht spazieren. Die beiden Frauen plaudern über ihren Alltag. Mama Pili Schwester wird bald heiraten.

Saida: Ehee. Lete habari. Tunasikia tu.

Mama Pili: Habari hakuna mwenzangu ila arusi ndiyo iko wiki ijayo.

Saida: Niambia saa!

Mama Pili: Nakuambia hivyo.

Saida: Ehee, wapi? Usiniambie mmekodi Arnautoglu⁶?

Mama Pili: Aah bwana wee! Arnautoglu nini! Mama alitaka kukodi Arnautoglu. Mimi nikakataa.

Saida: Eh?

Mama Pili: Kwa nini! Ndugu yangu wa mwisho mmoja tu anaolewa, kwa nini nikakodi Arnautoglu. Kina Hadija⁷ wakodi Arnautoglu na sisi vile vile? Aah wapi? Tumejitosa, tumeichukua Diamond Jubilee⁸.

Saida: Eh sema sasa. (*Wanacheka*)

Mama Pili: Na fanicha tumeagiza Nairobi.

Saida: (*Saida anaruka kwa furaha*) Watajua kama wameingiliwa. Nana alikwenda mpaka huko kuchagua?

Mama Pili: Tumeandika tu walete fanicha nzuri. Jina tu kama tumeagiza fanicha Nairobi linatosha. Tutatingisha Dar es Salaam. Nakuambia.

Saida: Ah mtaitingisha.

Mama Pili: Veli ya bi arusi basi, toba hee hee – (*Anapiga kofi*)

Saida: Kama ile aliyoiava Amne siku ya arusi yake? Ile mimi naliipenda.

Mama Pili: Aa veli gani ile. Veli tumeagiza Ulaya. Ulaya babu.

Saida: (*Anaruka ruka kwa furaha*) Niambie saa!

Mama Pili: Nakuambia hivyo. (*Anacheka*) Arusi ya juzi mwenzangu – Hm Po – Mimi naliona aibu. Bwana arusi na bibi arusi kama wameokotwa, kupendeza hawakupendeza, dhiki mashaka.

Saida: Veli hiyo hata kanzu yangu hii ghali - aibu tupu. (Uk. 52 - 54).

Mama Pili verabschiedet sich, da sie es mit den Vorbereitungen für die Trauung eilig hat. Saida reist ab.

2.2. 2. Onyesho la pili

Herr Omari befindet sich zu Hause. Jemand klopft an der Türe. Sein Freund Abudu

6 Zur britischen Kolonialzeit als „African Community Centre“ gebaut und nach dem griechischen Sponsor genannt. Er besaß Sisal-Plantagen.

7 Gemeint sind in dieser Aussage die „einfachen“ Leute. Die Edelfrau Hadija war aber die erste Frau des Propheten Mohammeds, die erste Person, die sich zum Islam bekannte und die Mutter von Fatma, die Frau des Khalifen Ali, dem Nachfolger des Propheten.

8 Die *Diamond Jubilee Hall* gehört der Aga Khan Ismaili Islamischen Gemeinde. Dieser Saal gilt als eher vornehmer Veranstaltungsort.

*kommt herein. Er hat eine Nachricht für Omari*⁹.

Omari: Karibu karibu. (*anaingia Abudu*) Pita tu, bwana, pita tu. (*Anataka kukaa juu ya kiti*). Aaah usikae hapo. Kiti kibovu. Kaa juu ya kitanda bwana. Jee habari za kwetu? Wote wazima?

Abudu: Ah! Hivyo hivyo. Saida yuko wapi? (*Kama anaogopa Saida atasikia*)

Omari: Amekwenda nyumbani. Hukumwona? Basi mmepishana, kajilawa hapa mapema. Nafikiri kaingia basi ya Nanji. Maana zile zinatoka mapema.

Abudu: Basi imekuwa heri kama kenda (akaenda) nyumbani. Mimi nimekuja makusudi yake.

Omari: Eh nini tena kilichozidi?

Abudu: Ah ndiyo (ndivyo) unavyojua tena. Binadamu ni binadamu bwana. Leo mzima kesho mgonjwa. Leo yupo kesho hayupo. Eh Bwana? Si jambo la ajabu. Si jambo la ajabu.

Omari: Kabisa, kabisa eh. (*Kimya. Kwa taratibu*). Lakini hukunimalizia.

Abudu: Ah kweli, kweli. Mambo haya yanasikitisha, yanahuzunisha, kwa hiyo mtu kusema mara moja tu hatari bwana.

Omari: Kabisa kabisa. Lazima yasemwe kwa taratibu na kwa upole. Hilo bila shaka.

Abudu: Ndiyo sawa sawa. (*Omari anamngojea lakini Abudu hasemi kitu*).

Omari: (*Kwa upole*) Eh ulisema vile kama nyumbani wagonjwa.

Abudu: Hapana si wagonjwa.

Omari: Si wagonjwa - aah - kama hiyo wazima.

Abudu: Hapana si wazima - si wazima kabisa. Ah! hapana si wazima.

Omari: Mpaka sasa bado mimi sijaelewa.

Abudu: Kwa kifupi nitasema kwamba mama yake Saida hayupo na sisi.

Omari: Amesafiri.

Abudu: Haswa - amesafiri - safari kubwa.

Omari: Safari kubwa? Kufanya nini?

Abudu: Bwana wake anamwita.

Omari: Hm, lakini sikujua mimi kama Mama Saida ana bwana.

Abudu: Kila mtu ana bwana - kila mtu, mzee na mtoto wote wanao Bwana. (*Kimya*)

Omari: Lini atarudi?

Abudu: Hatarudi - unasema nini bwana Omari? Unajua vyema kama mtu akiitwa na Bwana wake harudi.

Omari: Kweli kweli kwa hivyo alitaka mwanawe amuage sawa sawa kabisa. Basi atamwahi kabla hajaondoka.

Abudu: Ah amekwisha ondoka. Ilio baki sasa atawahi kumsindikiza.

Omari: (*Anafikiri*) Ameondoka, lakini atawahi kumsindikiza (*Haelewi*) (*Kimya*) Mimi Bwana Abudu sasa nakwenda kazini. Nina zamu ya saa tisa leo.

Abudu: Sasa wewe hutakuja mazishini?

Omari: Mazishini? Mazishi ni ya nani?

Abudu: Umekwisha sahau mara hii? Mazishi ya mama yake Saida.

Omari: Lakini umesema amekwenda safi... (*sasa anaelewa*) Aaah aah. Bila shaka, bila shaka. Ngoja nipite kazini dakika tano tu, niwaeleze huu msiba. Alaa si tunakwenda pamoja bwana?

Abudu: Mimi nimekuja kwa ajili ya kukuarifuni tu. Mimi nitarudi na basi ya saa tisa.

Omari: Tutakwenda pamoja, tutakwenda pamoja, na Saida ameisha fika sasa hivi. Twende. (*Wanaondoka*). (*Uk.57 - 59*).

9 Die umständliche Einleitung, die Abudu macht, gehört zur Kommunikationsweise der Waswahili. Siehe auch Karibu Mgeni von Graham Hyslop. (B.8.9.67.).

Langsam beginnt Omari zu ahnen, was Abudu ihm mitteilen möchte. Die Mutter Saidas ist tot.

2.2.3. Onyesho la tatu

Omari geht auf und ab, tief in Gedanken versunken. Er hält eine Nilpferdpeitsche in der Hand. Er hört jemanden kommen, setzt sich still auf den Rand seines Bettes und versteckt die Peitsche.

Saida : (Huku anacheka cheka) Hodi hodi wageni hao. Jee wenyewe wapo nyumbani? (Anavua buibui. Omari amenyamaza kimya) Wanakusalimu wote, baba, mama, wote wanakupa salamu.

Omari: Je, mama yako hajambo?

Saida: Sasa mzima kabisa. Na anakusalimu sana. Aliniuliza kama kwa nini hukwenda kumtazama? Mimi nikamwambia kama kazi zimekubana sana siku hizi. Utakapopata likizo utakwenda. Nimeleta zawadi kidogo. Ndizi hizi ametoa mama. Sehemu yako. (Uk. 60-61).

Saida hat auch Fisch mitgebracht. Sie essen sonst jeden Tag Reis. Sie möchte für ihren Mann heute Fisch und Bananen kochen. Omari schweigt.

Saida: Jee mbona unanitazama hivyo? (Kimya) Nimefanya nini eh? Kwa nini unanitazama namna hiyo? Sasa leo husemi? Mimi nakuuliza kama hutaki kujibu si basi. Kwani nani mwenye haja, mimi au wewe? (Kimya). Sasa una nini wewe eh? Umekuwa bubu? Kama nimekuudhi jambo sema. Sasa ukinyamaza tu namna hiyo mimi nitajuaje. Maana sisi binadamu kukosa ndiyo kwetu, lazima tuambiane. Nililokosa silijui. Narudi nyumbani, namkuta mume wangu ameninununia. Nikimwuliza hasemi. Nimekukosa nini? (Kimya) Najua kwa sababu nimekaa siku tatu badala ya siku mbili kwa mama. (Uso wa Omari unaonyesha kebehi. Maneno haya baada ya kumuudhi yanamchafua, lakini hasemi kitu.) Kama ungeliona siku nyingi siungaliniita basi. (Kimya) Kama hutaki kusema si basi, kila mtu anajua kunyamaza na mimi nitanyamaza. Kwani nikubembeleza wewe nani? (Ananyamaza, anajishughulisha na kupika. Omari anatazama tu. Bada ya muda anamjia Omari kwa hamaki) Sikiliza. Kama hutaki kuniambia usiniangalie. (Anachukua mwiko) Ukiendelea kunitazama, mwana wa haramu mimi, nitakupiga. (Kwa ukali) Nitakupiga usinitazame nakuambia. (Uk. 61 - 62).

Saida geht auf Omari mit dem Kochlöffel los. Er fängt ihre Hand ab. Er zeigt ihr die Nilpferdpeitsche, die er bis jetzt versteckt hielt. Er schlägt sie aber nicht. Er schaut sie an.

Omari: Mama yako amekufa siku tatu leo. Na tumemzika juzi. (Anamsukuma, Saida anapepesuka mpaka kitini, amebakia pale pale uso mikononi na huku amepiga magoti. Machozi anayataka lakini hayamjii. Amebaki anatemeka). (Uk. 63).

Saida ist fassungslos.

Saida: Kwa nini hunipigi. Nipige, niue. (Analetka kiboko, anampa mumewe) Nipige.

Huwezi? Unaniogopa, ndiyo unaniogopa. (*Anamcheka lakini sio kicheko cha furaha lakini kicheko cha mtu aliyojiwa*) Unaniogopa, ndiyo unaniogopa, kama huniogopi nipige. (*Anajaribu njia nyingine*) (Uk. 63).

Saida kommt zur Sache.

Saida: Nimelala nje siku tatu na mwanamume, unasikia, na mwanamume. Haya kama mwanamume kweli nipige. (*Anampa bakora anamshikisha mkononi, lakini Omari haichukui inaanguka chini*). Siyo mwanamume wewe. Mkeo anachukuliwa na watu na wewe umekaa tuu. Khanithi. Khanithi. (*Anaanza kulia na kucheka pamoja. Omari anakwenda mlangoni ili atoke nje. Saida anakimbia na kujitandaza mlangoni. Ukali wote umemuondoka. Anaomba kwa sauti nyenyekevu*). Tafadhali nipige ... tafadhali nipige. (*Anamkamata miguu. Omari anajitoa kwa taratibu.*)

Omari: Mimi sikupigi. (*Kimya*). Kama ukijaribu utawahi matanga. Wameanza kusoma jana. (*Omari anasema kwa .. taratibu. Kila neno linamwingia Saida kama msumari*) Kila mtu atafurahi kukuona. Baba yako (*Saida anaziba masikio huku anasema “nyamaza”*). Bibi yako.

Omari: Ndugu zako. Jamaa wote. (*Saida anauficha uso wake katika viganja vyake. Analia.*) (Uk. 63).

Er schließt die Türe und geht hinaus. Das Licht verlöscht langsam.

Tamati